## HUDUMA MBALIMBALI KUONGOZA MTOTO WAKO

Mtoto wako atakapofika shule au kituo cha uendeshaji wa bodi ya shule, ujuzi wake wa kifaransa itatathminiwa. Vilevile anaweza kutathminiwa hesabu na kufanyiwa mahojiano. Unaweza kuitwa kutoa maelekezo ili kuwasaidia wasimamizi wa shule kuelewa vizuri zaidi njia ya elimu ya mtoto wako na kutambulisha huduma ambazo mtoto wako atazohitaji.

Tathmini itawezesha kutambua kama mtoto wako atahitaji huduma za mapokezi na za msaada kwa mafunzo ya kifaransa ili kusoma kwa kutumia lugha hiyo na kufanikiwa katika masomo yote ya programu. Mtoto wako anaweza kupata huduma hizo darasani ya kawaida au darasani maalum kwa ajili ya kuunganisha wanafunzi wapya, mpaka waweze kufuata vizuri mafunzo inayotumia lugha ya kifaransa katika masomo yote.

Huduma za elimu za ziada zinatolewa shuleni ili kusaidia maendeleo ya wanafunzi na kuwaongoza katika njia zao za elimu. Huduma hizi zinaweza kutolewa na walimu ya marekebisho, wataalamu wa matibabu ya matatizo ya kunena, walimu wa nafsi au wanasaikolojia, kwa mafano.

Vilevile huduma zingine zinapatikana: usafiri wa kuhudhuria shule kwa hali maalum, huduma za uangalizi au kusimamia muda wa kula (shule ya chekechea na ya msingi), huduma ya mchukuzi wa chakula au ya kafeteria, n.k. Huduma hizi hata hivyo hazipo bure. Shule ya mtoto wako itakutaarifu kuhusu huduma zitoleazo.

## HUDUMA ZINAZOPATIKANA KWA AJILI YAKO PIA

Mafunzo ya jumla kwa ajili ya watu wazima inatoa baadhi ya programu kuitikia mahitaji na mategemeo ya watu wenye umri wa miaka 16 na kwenda juu kutokea tarehe 30 mwezi Juni ya mwaka uliopo. Mafunzo hiyo inatolewa na bodi za shule.

Huduma za kujifunza kifaransa inapatikana katika vituo vya elimu vya watu wazima.

Hatimaye, huduma za mapokezi, za marejeo, za ushauri na uangalizi zote zinatolewa ndani ya kila bodi ya shule. Huduma hizo zitakusaidia kutambua mradi wa mafunzo unaoendana na nia zao binafsi na kitaaluma.







## KARIBUNI QUEBEC NA SHULE YA SERIKALI YA LUGHA YA KIFARANSA

Hapa Quebec, asilimia 80 ya watu wanaongea kifaransa na kifaransa ni lugha ya serikali. Watoto wako wanapaswa kuhudhuria shule kwa lugha ya kifaransa hadi mwisho wa masomo yao ya sekondari.

Ni bure kuhudhuria shule na ni sharti kwa watoto wenye umri wa miaka 6 hadi 16. Shule inafungua mwisho wa mwezi Agosti au mwanzo wa mwezi Septemba na kwa kawaida inafungwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni. Wanafunzi wanahudhuria shule angalau siku 180 kila mwaka.

Mfumo wa elimu ni jukuma la Wizara ya Elimu na Elimu ya Juu. Usimamizi wa shule na mpangilio wa huduma za elimu kwa ajili ya elimu ya chekechea, elimu ya msingi na ellimu ya sekondari ni wajibu wa bodi za shule. Bodi za shule zimefikia 72 na zimenea mkoa wote wa Quebec.

## VIWANGO VYA ELIMU

### Elimu ya Chekechea
(Kabla ya umri wa miaka 6)

Elimu ya chekechea, au shule za watoto wadogo "maternelle", hutolewa siku nzima (masaa 4 na dakika 15 kila siku, kuanzia jumatatu mpaka ijumaa) kwa watoto ambao wameishafunga miaka 5 kabla ya tarehe 30 mwezi Septemba wa mwaka wa shule uliopo. Bodi za shule hutolea shule za watoto wadogo "maternelle" kwa watoto wenye umri wa miaka 4 katika baadhi ya maeneo.

Si lazima kuadhimisha shule ya chekechea "maternelle", lakini tunakadiria kwamba asilimia 98 ya watoto wenye umri wa miaka 5 wameandikishwa. Inawezesha, miongoni mwa mambo mengine, watoto wasioweza kuongea kifaransa kuanza kujifunza kwa kutumia lugha hili na kuwaandaa vizuri waanze shule ya msingi.

### Shule ya Msingi
(Kuanzia umri wa miaka 6 hadi 12)

Mafunzo ya shule ya msingi hutolea kwa masaa 5 kila siku, kuanzia jumatatu mpaka ijumaa, kwa wanafunzi ambao wamefunga angalau miaka 6 kabla ya tarehe 30 mwezi Septemba ya mwaka wa shule uliopo. Shule ya msingi kwa kawaida inaendelea kwa miaka 6.

### Shule ya Sekondari
(Kuanzia umri wa miaka 12 hadi 18)

Elimu ya sekondari hutolea kwa masaa 5 kila siku, kuanzia jumatatu mpaka ijumaa, kwa wanafunzi ambao wastani ya umri wao ni kati ya miaka 12 na 18. Shule ya sekondari kwa kawaida inaendelea kwa miaka 5. Wanafunzi wote wanafundishwa masomo yanayofanana kwa miaka miwili ya mwanzo. Baada ya miaka miwili hiyo, njia mbalimbali inapendekezwa kwa wanafunzi kulingana na shauku yao na ustadi.

## KUANDIKISHA KUENDA SHULE

Kuandikisha mtoto wako kuenda shule, unapaswa kuwasiliana na bodi ya shule inayosimamia shule za eneo lako au bodi ya shule ya mji unapoishi. Bodi ya shule itakufahamisha kuhusu taratibu za kufuata na michakato ya mapokezi, na itatoa maelekezo ya mawasiliano ya watu unaopaswa kuongea nao ili mtoto wako aandikishwe na aweze kuanzisha masomo katika shule yake mpya. Kujua jina la bodi ya shule ya eneo lako, unaweza kutafiti kwa tovuti la www.education.gouv.qc.ca kwa kubofya ikoni *Trouver une école*, chini ya kichwa cha *Actualités*. Unaweza pia kuwapigia simu huduma ya taarifa kwa jumla ya Wizara ya Elimu na Elimu ya Juu kwa nambari ya simu bila malipo 1 866 747-6626.

**Utahitaji kutoa baadhi ya hati wakati wa uandikishaji. Unapaswa kutoa hati halisi au nakala iliyothibitishwa yafuatayo:**

- Ithibati mbili ya makazi yako (wa mfano: bili ya umeme, bili ya huduma ya simu, barua ya serikali, mkataba wa kupangisha nyumba, n.k.).
- Ikiwa unaishi kwa watu au ndugu zako na huwezi kutoa ithibati yoyote ya makazi, yule mtu ambaye anakupa malazi anapaswa kujaza fomu fulani na kutoa thibati mbili ambayo inaonyesha makazi.
- Cheti chao cha kuzaliwa mtoto (kilichotafsiriwa kwa kifarasa au kiingereza).
- Hati za uhamiaji za wakati uliopo.

**Hati zifuatazo, zikipatikana, zinaweza kurahisisha uandikishaji:**

- Pasipoti isiyoishiwa muda wake.
- Hati inayothibitisha elimu ya watoto (kwa mfano: cheti cha matokeo).
- Kitabu cha chanjo.
- Tathmini mahsusi iliyotekelezwa na mwanasaikolojia au mtalamu wa matibabu ya matatizo ya kunena, kwa mfano.